
AUSCO

Programu ya Maelekezo ya Kitamaduni nchini Australia

# Elimu ya shule

Rahisi Kusoma

## Shule nchini Australia




Watoto katika Australia wanahitaji kwenda shule kati ya umri wa miaka ya 5 na 17.




Wao watatenda:

- shule ya msingi kwa miaka 6 au 7




- shule za sekondari kwa angalau miaka 4




Shule ya sekondari mara nyingi huitwa shule ya upili ya Australia.




Watoto wengi pia kwenda kwa shule ya kuchekechea kwa mwaka 1 kabla ya kuanza shule ya msingi.



Watoto wanawekwa katika masomo au viwango vya mwaka kulingana na umri wao.



Hii inaweza kuwa tofauti katika majimbo tofauti.




Kuna aina kuu 2 ya shule katika Australia:

- shule za serikali




- shule za kibinafsi

## Shule za serikali





Watoto wengi wataenda kwenye shule ya serikali.

Hizi zinaweza pia kuitwa shule za jumuiya.




Wewe huhitaji kulipa ada ya shule kama mtoto wako anaenda shule ya serikali.



Wewe unahitajika kulipia vitu kama vile:

- vitabu



- vitu vingine vya matumizi ya watoto darasani



- sare – nguo wanazohitaji kuvaa



- kambi na safari za utafiti – shughuli za watoto kufanya mbali na shule




Wewe unaweza kuongea na mtu katika ofisi ya shule kama unadhani hutawezikulipa kwa ajili ya mambo haya yote.

## Shule za kibinafsi




Shule za binafsi mara nyingi zinasimamishwa kwa:



- vikundi vya dini – Katoliki, Anglican, Lutheran, Protestant, Yahudi au Mwislamu



- vikundi vya huru




Ada kwa shule za binafsi zinaweza kuwa juu sana.

# Kujisajili katika shule




Wewe unaweza kupata msaada ili kuwasajilisha watoto wako katika shule kutoka kwake:

- mfanyikazi wa kesi



- au mshauri




Wewe utahitajika kuonyesha:

- nyaraka za safari yako





- kumbukumbu za chanjo ya mtoto wako – matibabu nayo kutoka kwa daktari au nursi  kuwazuia kupata wagonjwa




- ripoti au vyeti ambazo zinaonyesha shule au elimu ya mtoto wako tayari


# Kwenda shule




Mwaka wa shule huanza mwishoni mwa mwezi wa Januari na huishia mwezi wa Disemba.




Shule nyingi zina mihula 4.




Kunayo likizo ya shule kati ya mihula ya shule.




Shule hufungwa kwa likizo ya umma.





Watoto wengi huenda shule kwa masaa 6 kwa siku kutoka Jumatatu hadi Ijumaa.




Watoto lazima waenda shule. Hii ni sheria.



Ikiwa mtoto wako haendi shule, wewe unahitajika kutoa sababu kwa shule.




Shule inatarajia kuwa wewe utaandika kijibarua kidogo cha kuwafahamisha kwa nini mtoto wako alikuwa hafiki shuleni.

## Watoto katika shule Australia



Watoto kutoka asili mbalimbali huchanganyika pamoja shuleni.




Katika darasa, kunaweza kuweko na utofauti:

- rangi
- dini
- hali katika ghorofa ya jamaa



Shule nyingi huwachanganyishwa wavulana na wasichana katika darasa moja.



Kuna baadhi ya shule ambazo ni:

- za wavulana pekee



- za wasichana pekee

## Watoto ambao wanahitaji msaada wa ziada



Ikiwa mtoto wako anahitaji msaada wa ziada ili kujifunza Kiingereza wanaweza kwenda kwa Kiingereza kama masomo ya ziada ya lugha (English as an Additional Language - EAL).



Kwa kawaida masomo ya EAL hufanyika katika shule ya mtoto wako.





Watoto walio mahitaji maalumu wana haki sawa na watoto wengine.

Mtoto wako anaweza kuwa na mahitaji maalum ikiwa kama anao:



- ulemavu wa kimwili



- ulemavu wa kiakili



- tatizo la kusikia au wao ni viziwi



- tatizo la macho au wao ni vipofu



- ulemavu wa kimasomo



- tatizo kwa sababu ya tabia zao



Watoto wenye mahitaji maalum huwa ni pamoja na masomo katika shule za kawaida.



Pia kuna shule kwa watoto wenye mahitaji maalum tu.

# Shule zipo vipi



Katika shule, watoto wanaitwa wanafunzi.



Walimu katika shule nchini Australia huwa kutia moyo wanafunzi wao ili:

- wafikirie wenyewe



- kuchambua – kuchunguza kwa nini mambo yanatokea



Walimu hawatarajii wanafunzi kujifunza kwa kukumbuka mambo tu.



Wanafunzi hushiriki katika darasa na:


- kuuliza maswali



- kuzungumza juu ya mambo



- kujaribu kazi na shughuli tofauti za kujifunza




Wanafunzi wanaweza kushiriki hata kama hawazungumzi Kiingereza sana.



Wanafunzi wanahimizwa kushiriki katika aina mbalimbali ya shughuli za shule:

- lugha – kusoma na kuandika



- hisabati – matumizi ya nambari



- michezo



- muziki



- safari za utafiti na kambi – safari mbali na shule kuwapatia wanafunzi uzoefu ziada kujifunza



Shule zote hufunza mfumo wa elimu wa Australia.
[www.australiancurriculum.edu.au](http://www.australiancurriculum.edu.au)

# Wazazi na shule za watoto wao



Shule wanataka wazazi kuwa sehemu ya elimu ya mtoto wao.



Wewe unaweza:

- kwenda kwenye mikutano na kuzungumza na mwalimu wa mtoto wako




- kuhakikisha kuwa mtoto wako anakamilisha kazi zao za shule pamoja na kazi za ziada za nyumbani



- kwenda kwenye matukio ya shule kama vile
  - matamasha na michezo
  - siku za michezo



Ni sawa kwako wewe kuzungumza na mkuu wa shule kuhusu:

- motto wako na jinsi anavyojifunza
- jinsi mambo yanavyoendelea shuleni



Mwalimu mkuu ni kiongozi wa shule.



Unaweza kupata habari zaidi kwenye tovuti ya Idara ya Elimu na Mafunzo (Department of Education and Training). www.education.gov.au

## Huduma ya utunzaji wa watoto na mafunzo ya mapema



Utunzaji wa mtoto na kujifunza mapema huwapa watoto wadogo nafasi ya:


- kujifunza na kuendeleza mahali salama



- kucheza na kuzungumza na watoto wengine



- kuelewa hali ya moyo yao, na hisia kama vile hisia ya watu wengine



Pia huwapa wazazi ambao wana kazi fursa ya kwenda kufanya kazi.



Unaweza kupata maelezo zaidi juu ya huduma za watoto na huduma za kujifunza mapema kwenye tovuti ya MyChild.
[www.mychild.gov.au](http://www.mychild.gov.au)

Australian Government
Department of Social Services

Inaletwa kwako na Shirika la Uhamiaji la Kimataifa kwa niaba ya Idara ya Huduma za Jamii nchini Australia

IOM • OIM